



## **Mwanamke yeyote atakayeolewa bila idhini ya walii wake, basi ndoa yake ni batili" Akasema hivyo mara tatu "Ikiwa atamuingilia basi mahari yake ndio itakuwa kwa ajili ya kile alichokifanya kwake, na ikiwa watazozona basi kiongozi ndiye msimamizi wa asiyekuwa na msimamizi**

Kutoka kwa Aisha -radhi za Allah ziwe juu yake- amesema: Amesema Mtume -rehema na amani ziwe juu yake-: "Mwanamke yeyote atakayeolewa bila idhini ya walii wake, basi ndoa yake ni batili" Akasema hivyo mara tatu "Ikiwa atamuingilia basi mahari yake ndio itakuwa kwa ajili ya kile alichokifanya kwake, na ikiwa watazozona basi kiongozi ndiye msimamizi wa asiyekuwa na msimamizi".

[Sahih] [Imepokelewa na Abu Daud, Tirmidhiy, Ibn Majah na Ahmad]

Alitahadharisha Mtume rehema na amani ziwe juu yake mwanamke kujiozesha mwenyewe pasina idhini ya walii wake, nakwamba ndoa yake ni batili, na hilo alilikariri mara tatu, kana kwamba haijatendeka. Akimuingilia huyu aliyemuoa pasina idhini ya walii wake; hapo mahari kamili itakuwa ni haki yake, kwa lile tendo la ndoa alilolipata katika tupu yake. Kisha wakizozana mawalii kuwa ni nani mwenye haki ya kufungisha ndoa (na daraja zao zikawa ni sawa) ndoa itafungishwa na yule atakayetangulia miongoni mwao, ikiwa huyu anamtazamo mzuri katika masilahi ya mwanamke huyo, walii akikataa kumuoza basi hapa mwanamke atakuwa ni sawa nakwamba hana walii; hapa kiongozi au kadhi na mfano wao ndio watakuwa mawalii wake, na vinginevyo hakuna uwalii wa kiongozi anapokuwepo walii.

<https://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/58067>

